

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA WAZIRI MKUU  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO**

**SHULE YA SEKONDARI HOROMBO.  
S.L.P 186,  
MKUU – ROMBO  
TAREHE.....**

**SIMU NA. - 0784 -347795  
0652-190906 -MKUU WA SHULE**

**0782921188  
0756455756 – MAKAMU WA MKUU WA SHULE**

**Kumb. Na. HOSS/ADM & TRAN/VOL.IV.....**

**MZAZI /MLEZI WA MWANAFUNZI**

.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI HOROMBO KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021- KUTWA**

**1.0 UTANGULIZI.**

Ninayo furaha kukujulisha kwamba umechaguliwa kijiunga na Elimu ya Sekondari kidato cha kwanza shule ya Sekondari Horombo iliyopo wilaya ya Rombo Mkoani Kilimanjaro.

Shule ipo kilometra 5 toka kituo cha mabasi mkuu Wilayani. Ni imani yangu kuwa ufikapo shulenii utatumia vizuri nafasi hii uliyotunukiwa na Taifa lako kusoma kwa bidii na maarifa masomo yote yanayofundishwa hapa shulenii ili kujiletea maendeleo yako binafsi, kwa familia yako na Taifa kwa ujumla. Mazoezi na majaribio utakayoyafanya darasani ukumbuke ni sehemu ya mitihani yako ya mwisho ya kidato cha nne. Hivyo unapokuja shulenii lengo lako liwe ni kujifunza kwa bidii ili kupata elimu bora na endelevu.

Aidha, tunaamini kuwa ili ufanikiwe kimasomo lazima uwe na nidhamu ya hali ya juu. Sheria na kanuni za shule nimekufungashia soma kwa makini na ujue kuwa **kumcha Mungu ni chanzo cha maarifa**.

**2.0 MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA HAPA SHULENI**

Ukiwa hapa shulenii utasoma masomo yote ya sayansi na sanaakwa miaka minne ambayo ni:- PHYSICS, CHEMISTRY, BIOLOGY, CIVICS, KISWAHILI, ENGLISH LANGUAGE, GEOGRAPHY, BASIC MATHEMATICS, HISTORY PHYSICAL EDUCATION. Aidha unaweza kusoma somo moja la ziada kati ya LITERATURE IN ENGLISH, ICS (INFORMATION AND COMPUTER STUDIES)AU PHYSICAL EDUCATION kuanzia kidato cha tatu.

### **3.0 KUFUNGUA SHULE**

Shule itafunguliwa tarehe 11 Januari 2021. Unatakiwa ufile shulen i siku ya Jumatatu saa 1:30 asubuhi bila kukosa ukiwa na mzazi/mlezi.

Aidha siku ya kufungua kutakuwa na kikao kifupi cha wazazi/walezi wa kidato cha kwanza mwaka 2021 kitakachoanza saa 2:00 asubuhi ndipo suala la usajili wa wanafunzi lifuate. Ni muhimu sana usikose na mwanafunzi hatasajiliwa bila kufika na mzazi/mlezi.

### **4.0 MAHITAJI MUHIMU**

#### **4.1. SARE YA SHULE KWAWASICHANA (KUTWA)**

- (i) Sketi mbili (2) kitambaa cha cotton (grade I) rangi imeambatanishwa.
- (ii) Blauzi 2 tetron nyeupe mikono mifupi (TOMATO)
  - (iii) Tai ndefu ya rangi ya ya sketi (iv) Sweta mbili rangi ya sketi.
- (v) T – Shirts za michezo
- (vi) Viatu vyeusi vya ngozi, visigino vifupi, vyenye kamba (gidamu) jozi 2
- (vii) Jezi ya michezo, raba, soksi ndefu na skin tight ndefu.(kwa ajili ya somo la physical education)
  - (viii) Soksi nyeupe mpya (TOMATO)

#### **SARE YA SHULE KWA WAVULANA (KUTWA)**

- (i) Suruali mbili (2) kitambaa cha cotton rangi imeambatanishwa (grade I)
- (ii) Shati 2 tetron nyeupe mikono mifupi (TOMATO)
- (iii) Tai ndefu ya rangi ya suruali
- (iv) Sweta mbili rangi ya suruali
- (v) T – Shirts za michezo
- (vi) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi na kamba (gidamu) jozi 2
- (vii) Jezi ya michezo, raba, soksi ndefu .(kwa ajili ya somo la physical education) (viii) Mkanda mweusi wakuvalia suruali,usiwe na maandishi na uwe na bakoli ya kawaida (ix) Soksi nyeusi mpya jozi mbili.

#### **NB:**

- (i) Mashono –Wavulana suruali ishonwe pana isiwe chini ya inchi 15 mzunguko wa chiniNi **marufuku kushona suruali iliyobana** (kimodo) na zingatia aina ya kitambaa kilichoambatanishwa.
  - Wasichana sketi ishonwe ndefu isiyopungua inchi 15 kutoka gotini kwenda chini,mshono ni marinda boksi.
- (ii) Sweta – liwe jipya la special na sio vinginevyo
- (iii)Ufikapo shulen i uwe umevaa sare kamili vinginevyo hutapokelewa
- (iv) Wanafunzi wa Kiislamu wanaruhusiwa kuvalia Hijabu shulen i hivyo ishonwe kwa mujibu wa sheria na sketi iwe ndefu isiyopungua inch 6 kutoka kwenye kiatu

#### **4.2. VIFAA VYA USAFI NA KULIA CHAKULA**

Kila mwanafunzi anatakiwa aje na vifaa vifuatayo siku ya kufungua ,vifaa hivi vitakaguliwa kabla ya kumsajili mwanafunzi.

- (i) Bakuli la cello lenye mfuniko la plastiki, kikombe cha plastiki na kijiko. (ii) Vifaa vya usafi tutajadiliana kwenye kikao.

#### **4.3. VIFAA VYA DARASANI**

- (i) Madaftari 11makubwa (counter books) quire 3
- (ii) Madaftari 11 madogo ya mazoezi
- (iii) Kalamu za kutosha (black/blue)

- (iv) Mathematical set 1
- (v) Dictionary (kamusi ya Kingereza -Kingereza)

#### **4.4.AFYA YA MWANAFUN ZI**

Hakikisha kuwa mwanaao anakuja shulenii na taarifa sahihi ya vipimo vyote toka kwa daktari aliyempima, vinginevyo hatutapokea malalamiko ya magonjwa ambayo hayakupimwa.

- (i) Jaza fomu C (imeambatanishwa)
- (ii) Jaza fomu D (imeambatanishwa)
- (iii) Jaza fomu E (imeambatanishwa)

Siku ya kumleta mwanaao shulenii uje na fomu C, D na E zikiwa tayari zimekamilika na **risiti ya malipo ya upimaji kutoka kituo au Hospitali ya serikali** na sio vinginevyo.

**NB:** Aidha kila mwanafunzi awe na kadi ya bima ya afya ( ICHF/NHIF AU NYINGINE INAYOTAMBULIKA NA SERIKALI) kuondoa usumbufu shulenii endapo ataugua kwa ghafla .

#### **5.0 MICHANGO YA CHAKULA**

Michango yote ya chakula na maendeleo ya shule itatokana na makubaliano ya kikao cha wazazi kitakachofanyika tarehe 11/01/2021

.....  
**ELINE .S. LEMA  
MKUU WA SHULE.**

HOROMBO SECONDARY SCHOOL,  
P.O BOX 186,  
**MKUU – ROMBO.**

DATE .....

Ref. No. TSS/JI/.....

To the Medical Officer in charge,  
(Hospital /Health Centre)

.....  
.....  
.....

### **REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

Please examine ..... (Name of student) who has been selected to join this school for his/her fitness as a student in the following areas:-

(To be completed by Medical Officer)

1. Eye site .....
2. Hearing .....
  
3. Specimen:-
  - (i) Stool: .....
  - (ii) Urine .....
  - (iii) Blood: .....
  
4. Pregnancy .....
5. Asthma .....
6. Tuberculosis .....
7. Others .....

### **MEDICAL CERTIFICATE:** **(To be completed by medical officer)**

I have examined the above student and consider him/her Physically fit/unfit as a student

Date ..... Signature .....

Station ..... Designation .....

**NB:** I request that this form has to be returned to school in envelope.

**OFISI YA WAZIRI MKUU  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
SHULE YA SEKONDARI HOROMBO.**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA ELIMU YA SEKONDARI KIDATO CHA KWANZA 2021**

Fomu hii ijazwe na mzazi/mlezi pamoja na mwanafunzi aliyechaguliwa kuingia kidato cha kwanza kisha mwanafunzi ailete shulenii baada ya kuthibitishwa na mtendaji wa kijiji alichotoka.

**1. Mwanafunzi**

Mimi ..... kwa hiari yangu ninakubali/sikubali nafasi niliyopewa ya kuingia kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Horombo. Nitakuwa tayari kufuata sheria na taratibu zote za shule wakati wote nikiwa mwanafunzi wa shule hii.

Saini ya mwanafunzi: .....

Tarehe .....

**2. Mzazi/mlezi**

Mimi ..... Mzazi/mlezi wa ..... nimekubali/sikubali nafasi aliyopewa mtoto wangu na kwamba muda wote akiwa mwanafunzi wa shule ya Sekondari Horombo anapaswa kufuata sheria na taratibu zote za shule. Pia nikiwa ni mzazi/mlezi wake naahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi yake na gharama zote zitakazomwezesha kusoma bila vikwazo hadi kumaliza masomo yake.

Saini ya mzazi/mlezi .....

Tarehe .....

**3. Afisa Mtendaji Kata.**

Mimi ..... mtendaji wa kata ..... ninathibitisha kuwa ndugu ..... ni mzazi/mlezi wa mtoto huyu aliyechaguliwa kuingia kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Horombo mwaka 2021. Na kwamba anawajibika kumtolea mwanaye michango ya chakula kwa mujibu wa maamuzi ya kikao cha wazazi.

Saini ya Afisa Mtendaji kata.....

Tarehe na muhuri wa Afisa Mtendaji kata .....

**OFISI YA WAZIRI MKUU  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA SHULE  
YA SEKONDARI HOROMBO.  
TAARIFA BINAFSI ZA MZAZI/MLEZI**

**Ijazwe na mzazi/mlezi**

Jina kamili la mzazi/mlezi .....

1. Kazi yake .....
2. Nyumbani kwake .....
3. Anwani ya nyumbani ..... Kijiji  
 ..... kata ..... Wilaya ..... Mkoa  
 ..... Anwani ya mahali pa kazi  
 ..... (kama ipo)
- Namba ya simu ya mkononi..... ( kama ipo)
- Mji .....
4. Dini ya mzazi/mlezi ..... dhehebu .....
5. Dhehebu unalotaka mtoto wako alelewé .....
6. Anwani kamili ya nyumbani atakakokwenda mwanafunzi wakati wa likizo  
 .....  
 .....
7. Anwani ya kazini kama ni tofauti na ya hapo juu .....
8. Jina la mwanafunzi na tarehe ya kuzaliwa kama ilivyo kwenye cheti cha kuzaliwa au cha ubatizo.  
 .....
9. Mwanafunzi akiwa hapa shulenii, anaweza kutembelewa na watu wafuataao  
 (i) ..... (ii) ..... (iii) ..... kama mimi  
 mwenyewe nitashindwa kufika na sio vinginevyo..
10. Mimi ..... Mzazi/Mlezi ninathibitisha kuwa taarifa za hapo  
 juu ni sahihi.

Saini ..... Tarehe .....

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO.  
SHULE YA SEKONDARI HOROMBO.  
SHERIA ZA SHULE**

**1. HESHIMA NA UTII**

- (i) Ni lazima kila mwanafunzi aheshimu na kutii viongozi wote waliowekwa juu yake ambao ni Walimu, Wafanyakazi wasio walimu, serikali ya wanafunzi na wale wote waliomzidi umri.
- (ii) Ni lazima kila mwanafunzi asimame na kusalimia viongozi na wakuu wote anaokutana nao shulenii.
- (iii) Ni lazima kila mwanafunzi kutii mara moja na kuwahi mahali anapotakiwa wakati asikiapo kengele au wito mwingine wowote ule.
- (iv) Ni lazima kila Mwanafunzi atii maagizo kwanza kabla ya kujenga hoja ya kujitetea.
- (v) Ni MARUFUKU kwa Wavulana na wasichana kwenda sehemu za maficho zilizokatazwa wakiwa eneo la shule.

**2. MAHUDHURIO NA KUWAHI**

- (i) Ni lazima kila mwanafunzi awepo shulenii muda wote wanapotakiwa.
- (ii) Ni lazima kila mwanafunzi ahudhurie katika vipindi vyote ndani na nje ya darasa, kwa kuwahi bila kukosa.
- (iii) Mwanafunzi akikosa shule kwa zaidi ya siku 3 mfululizo katika muhula mmoja bila sababu zenyekukubalika na shule anaweza kusimamishwa masomo kama adhabu.
- (iv) Mwanafunzi haruhusiwi kuondoka shulenii bila ruhusa ya Mkuu wa shule/Makamu au mwalimu wa zamu.

**3. UVAAJI WA SARE ZA SHULE**

- (i) Ni lazima kila mwanafunzi awe msafi awapo shulenii au nje ya shule.
- (ii) Sare ya shule ni lazima ivaliwe wakati wote mwanafunzi akiwa shulenii. Ni lazima iwe imefuliwa na kupigwa pasi kila siku.
- (iii) Mwanafunzi haruhusiwi kuweka urembo wa aina yoyote katika sare ya shule.
- (iv) Mashati na blauzi ni lazima yachomekewe na vishikizo vyote viwepo na kufungwa.
- (v) Nywele ziwe fupi zilizochanwa na nadhifu.
- (vi) Viatu viwe safi na nyeusi vya ngozi, vyenye gidamu.
- (vii) NI MARUFUKU kwa mwanafunzi kuva .
  - (a) Kilemba au kofia
  - (b) Mapambo mikononi au kichwani
  - (c) Kuchora kwa kutumia rangi au kitu chochote chenye ncha kali katika mwili wake (Tattoos).
  - (d) Mikufu shingoni
  - (e) Nywele za bandia au viatu vya ghorofa.
  - (f) Pete vidoleni.
  - (g) Hereni masikioni

- (h) Vipuli puanii
- (i) Kanda mbili n.k
- (viii) Mwanafunzi HARUHUSIWI
  - (a) Kuwa na ndevu
  - (b) Kuwa na kucha ndefu
  - (c) Kupaka kucha au nywele au macho au mdomo rangi
  - (d) Kukaanga nywele (kuweka nywele dawa)
- (ix) Ni marufuku kabisa kuvalaa kipedo au mLegezo shulenii ,hutavumiliwa.

#### **4. LUGHA YA MAWASILIANO**

- (i) Mwanafunzi kwa wanafunzi na walimu watawasiliana kwa lugha ya KIINGEREZA isipokuwa katika somo la Kiswahili na Dini ikibidi.
- (ii) wanafunzi watawasiliana na watu wengine kwa lugha ya Kiswahili ikibidi.
- (iii) Ni MARUFUKU kwa mwanafunzi kuwasiliana kwa lugha nyingine yoyote awapo kwenye maeneo ya shule.
- (iv) Lugha chafu au matusi HAYARUHUSIWI SHULENI KABISA.

#### **5. USAFI WA MAZINGIRA**

- (i) Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuweka eneo la shule na majengo ya shule katika hali ya Usafi
- (ii) Vyoo na ukumbi wa chakula ni lazima viwe safi na vitumiwe ipasavyo.
- (iii) Uchafu/takataka ni lazima vitupwe mahali panapostahili na iwe desturi yako.
- (iv) Ni marufuku kuandika – andika kwenye kuta za majengo, viti na madawati.
- (v) Iwapo Mwanafunzi amekatazwa kufanya kazi yeyote kwa sababu za kiafya UTHIBITISHO wa maandishi ya Daktari wa Hospitali ya Serikali unahitajika.

#### **6. KUTOKA NJE YA MIPAKA YA SHULE.**

- (i) **Ni MARUFUKU** kwa mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule wakati wa masomo au shughuli nyingine za kishule bila ya ruhusa ya maandishi (Pass or permitte sheet). (ii) Mwanafunzi anaporuhusiwa kutoka nje ya eneo la shule ni MARUFUKU kutembelea sehemu zifuatazo:-
  - (a) Nyumba za kulala wageni
  - (b) Nyumba za starehe
  - (c) Vilabu vya pombe
- (iii) **Ni MARUFUKU** kwa mwanafunzi kutembelea sehemu zifuatazo shulenii isipokuwa kwa kibali au sababu maalumu:-
  - (a) Chumba cha walimu (staff - room)
  - (b) Nyumba za walimu au Wafanyakazi wasio Walimu
  - (c) Ofisi na stoo ya shule
  - (d) Jikoni
  - (e) Maabara (wakati usio wa vipindi)
  - (f) Sehemu zenye mashamba na mifugo kama hausiki.

## **7. IBADA**

Kila mwanafunzi ana haki ya kuabudu kwa kadiri ya imani yake bila kubughudhiwa na mtu yejote. Mwanafunzi ataruhusiwa kusali nje ya shule siku za ibada kwa kuzingatia taratibu za kuondoka shulenii kibali maalumu.

## **8. MICHEZO**

- (i) Ni lazima kila Mwanafunzi ashiriki katika michezo inayofanyika shulenii.
  - (ii) NI MARUFUKU kwa mwanafunzi kuchezea vilabu vya michezo nje ya shule.
- Ni lazima mwanafunzi avae nguo za michezo anapokuwa uwanjani na siyo sare ya shule

## **9. ADHABU ZINAZOTOLEWA NA SHULE**

Adhabu zinazotolewa shulenii kwa wanafunzi waliokiuka sheria za shule ni:-

- (i) Kuonywa kwa Mdomo au Maandishi
- (ii) Kupiga magoti kwa muda
- (iii) Kufanya kazi za nje
- (iv) Kuchapwa viboko ( kwa idhini ya mkuu wa shule)
- (v) Kufikishwa katika kamati ya Nidhamu kwa hatua kali za kinidhamu.

## **10. MAKOSA YA KUFUKUZWA SHULE**

- (i) Wizi
- (ii) Ulevi wa pombe au madawa ya kulevyaa kama vile Uvutaji bangi/sigara, cocaine, Mirungi, kuberi n.k
- (iii) Kugoma, kuchochaea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au jamii. (iv) Kutoheshimu Bendera ya Taifa, Picha ya Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania na Makamu wake, na Fedha ya Tanzania. (v) Uasherati na ushoga
- (vi) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule
- (vii) Kuoa au kuolewa
- (viii) Kupata mimba au kutoa mimba
- (ix) Kukataa adhabu iliyotolewa na uongozi wa shule kwa kisingizio chochote.
- (x) Kupigana na kumshambulia mtu yejote au kuzomea.
- (xi) Kutohudhria masomo kikamilifu
- (xii) Mwanafunzi kukutwa na kutumia simu ya mkononi shulenii.

.....  
**ELINE .S. LEMA**  
**MKUU WA SHULE**